BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

# TNMC HABARI

Jarida la Mwezi

Januari, 2024

Toleo N0. 004

HALIUZWI

www.tnmc.go.tz @tnmchabari



**4142**

Ni jumla ya watahiniwa waliofanya mtihani

# Watahiniwa 2099 Wafaulu Mtihani wa Usajili, Leseni

...Ni ngazi ya SHAHADA, STASHAHADA, ASTASHAHADA.

Habari UK 01.

# Baraza latoa adhabu kwa wauguzi, wakunga Nane.



## Adhabu zatolewa

Wapo waliosimamishwa kutoa Huduma, wengine wapewa Kalipio kali

## Msimamo wa TNMC

Wauguzi, wakunga watakiwa kuzingatia Sheria, kanuni ya Taaluma ya Uuguzi, Ukunga

Habari UK 02.

# TIMU YA WAHARIRI

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

## MHARIRI MKUU

Bi.Agnes Mtawa

## MHARIRI

Mwakapiso Ndimmyake

## WARATIBU

Irene Chilewa na Rose Mhando

## MSANIFU JARIDA

Ezekiel M Nyalusi

P.O BOX1736 DODOMA
TEL.022-212133975 Fax.022-2133975 Mobile:0786785947

@tnmchabari www.tnmc.go.tz Info@tnmc.go.tz

# TNMC Yatangaza Matokeo ya Usajili na Leseni

***Na Mwandishi wetu.***

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) limetangaza Matokeo ya Mtihani wa Usajili na Leseni uliofanyika Tarehe 29.12.2024.



***Msajili wa Baraza Bi.Agnes Mtawa, akitoa taarifa ya Matokeo ya Mtihani wa Usajili na Leseni uliofanyika Tarehe 29.12.2024.***

Akitangaza Matokeo hayo katika Ofisi za Baraza Jijini Dodoma, Msajili wa Baraza Bi.Agnes Mtawa, amesema, Mtihani huo uliofanyika katika vituo nane (8) ambavyo ni Taasisi ya Afya na Sayansi Shirikishi Tandabui-Mwanza, Taasisi ya Afya na Sayansi Shirikishi-Mbalizi, Chuo Kikuu cha Kumbukumbu Stephano Moshi-Kilimanjaro, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (St.John) – Dodoma, Chuo Kikuu cha Kampala-Dar es Salaam, Chuo cha Biashara -Dodoma (CBE) na Chuo cha Tabora Polytechnic.

Jumla ya watahiniwa 2099 (50.7%) walifaulu mtihani huo kati yao watahiniwa 346 (72%) ni ngazi ya Shahada ya Uuguzi, 1737 (48%) ni Stashahada ya Uuguzi na Ukunga na watahiniwa 16 (30.8%) ni Astashahada ya Uuguzi na Ukunga.Watahiniwa 2043 (49.3%), walifeli mtihani huo, kati yao 136 (28%) ni ngazi ya Shahada (Digree) ya Uuguzi, 1871 (52%) ni Stashahada (Diploma) ya Uuguzi na Ukunga na 36 (69.2%) ni Astashahada( Cheti) ya Uuguzi na Ukunga.

*"Maswali ya mtihani huu yalichambuliwa kwa ngazi ya mafunzo ili kuona hali ya ufaulu wa watahiniwa katika maeneo ya umahiri uliopimwa kwa kuzingatia orodha ya vipimo vya umahiri na watahiniwa wengi walionekana kushindwa na kuwa nauelewa mdogo katika maeneo ya Misingi ya Uuguzi (Basic/ Fundamentals of Nursing), tiba upasuaji na magonjwa ya dharura na mahututi (Medical Surgical Nursing and intensive care), Afya ya Mama na Mtoto (Midiwifery and Child Health), Afya ya Akili (Mental Health Nursing)"* alitanabaisha Msajili huyo.

Aidha, ameongeza kuwa, Katika Mtihani huu, hali ya Ufaulu inaonesha kunaongezeko la asilimia 4.7 ukilinganisha na mtihani uliofanyika mwezi Disemba, 2022 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 4.6. Ngazi ya Shahada ni 71%, Ngazi ya Stashahada ni 71% Ngazi ya Astashahada ni 56%

Akihitimisha tarifa yake, Msajili Mtawa, amesema, Baraza litatoa mrejesho kwenye vyuo vya Uuguzi na Ukunga na vituo vya utarajali kuendelea kuongeza usimamizi wanafunzi ili kujifunza zaidi katika maeneo hayo.

Baraza kwa kushirikiana na viongozi wa Uuguzi na Ukunga katika Mikoa na Wilaya (Supervisory Authority) kuendelea kuimarisha ufuatiliaji wa vyuo vya Uuguzi na Ukunga na usimamizi wa wanafunzi katika maeneo ya kujifunza kwa vitendo

Baraza kufuatilia vyuo vya Uuguzi na Ukunga ili kubaini hali halisi ya uwepo wa mazingira bora ya ufundishaji katika Hospitali na vyuo.

Kufanya ufuatiliaji wa vituo vya mafunzo ya utarajali na vyuo ambavyo watahiniwa wameonyesha kupata ufaulu wa kiwango cha chini ili kubaini changamoto zinazowakabili.

Wauguzi na wakunga hao wanatarajiwa kukabidhiwa vyeti vya usajili na leseni na kutambuliwa kama wataalam wa kada hizo kwanye Mahafali maalum ya kitaaluma yanayotarajiwa kufanyika Jijini Dodoma 23/02/2024

# Baraza Latoa Adhabu kwa Wauguzi, Wakunga Nane.



***Mwenyekiti wa Baraza profesa Lilian Mselle (katikati), Msajili wa Baraza Bi.Agnes Mtawa(kushoto), wakiongoza kikao cha 218 kilichofanyika jijini Dodoma.***

***Na Ezekiel Nyalusi.***

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania likiwa ni Mamlaka ya kisheria yenye jukumu la kusimamia taaluma ya Uuguzi na Ukunga Tanzania, mapema mwezi Januari mwaka huu, liliwahoji na kutoa hukumu kwa wakuguzi na wakunga nane kutoka maeneo mblimbali nchini kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Akizungumza na Wanahabari wakati wa kikao cha 218 cha Baraza, Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini Prof. Lilian Mselle, Alibainisha kuwa, Baraza limesikiliza mashauri manne (4) ya tuhuma za uvunjifu wa maadili yaliyowahusisha wauguzi na wakunga 08 kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010.











# Wauguzi 81 Watunukiwa Vyeti, Leseni za Kitaaluma



*Wahitimu wa kozi ya Uuguzi na Ukunga wakiapa wakati wa Mahafali yaliyofanyika jijini Dodoma*

***Na Ndimmyake Mwakapiso.***

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) limeandaa Mahafali kwa Wahitimu wa kozi za Uuguzi na Ukunga waliofaulu Mtihani wa Usajili na Leseni uliofanyika tarehe 07/09/2023.

Mahafali hayo ya tisa yamefanyika Jijini-Dodoma, ambapo wauguzi na wakunga wapatao 81 wametunukiwa vyeti pamoja na leseni za kutambuliwa rasmi kama wataalam wa kada hizo.

Akizungumza wakati wa Mahafali, Mgeni rasmi ambaye ni Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa, amewapongeza wauguzi na wakunga hao kwa hatua waliyoifikia ya kuaminiwa na Baraza na kuwataka kwenda kuhudumia jamii kwa kutanguliza Utu.
*"Tujikite katika kutoa Huduma bora kwa jamii, leo Baraza limeridhika na viwango vya taaluma yenu kwa kuwapa leseni na cheti cha usajili wa taaluma, mkaihudumie jamii kwa kufuata Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kilasiku, mkizingatia kuwa kazi yetu ni kazi maalum kwa watu maalum ambayo inahitaji upendo na utayari wakati wote"* alisema Bi. Mtawa

Naye Mwanasheria wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania George Shilla, amewasihi wauguzi na wakunga kuzingatia Sheria ya Uuguzi na Ukunga wanapokuwa kazini ili kuepukana na adhabu ambazo zipo kwa mujibu wa Sheria.

Kati ya Watahiniwa 81 waliohitimu katika Mahafali hayo ya tisa ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania 32, ni wa ngazi ya Astashahada wakati Shahada ni wahitimu 49






# Wauguzi, Wakunga 142 Wanuafaika na Mafunzo ya Maadili.



***Wauguzi na wakunga wa Hospitali ya Taifa ya Mirembe wakiwa na Afisa Muuguzi Mbobezi Kitengo Cha Upasuaji Bi. Salome Kassanga, baada ya Mafunzo ya ushiriki katika chumba***

***Na Ezekiel Nyalusi.***

Jumla ya Wauguzi, wakunga na watarajali 134 wamenufaika na Mafunzo ya Maadili pamoja na uhamasishaji kuhusu Maadili katika Hospitali tatu ambazo ni Hosiptali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali tanzu ya Mloganzila na Hospitali ya Tumbi Kibaha mkoni Pwani.

Mkurugenzi wa Usajili, Leseni na Maadili Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Jane Mazigo, ndiye aliyeratibu na kuendesha mafunzo hayo yenye lengo la kuwajengea uwezo wauguzi na wakunga ili waweze kutoa huduma bora kwa jamii.

Katika hatua nyingine, Baraza pia limeendesha Mafunzo ya kushiriki namna bora ya utoaji huduma katika chumba cha upasuaji kwa Wauguzi na Wakunga nane (08) katika Hospitali ya Mirembe Jijini Dodoma.
Akitoa mafunzo hayo, Afisa Muuguzi Mbobezi Kitengo Cha Upasuaji Bi. Salome Kassanga, amewataka Watumishi hao kuyazingatia yale waliyojifunza ili kuhakikisha jamii inapata huduma iliyo bora na salama.

Kwa upande wake Muuguzi Kiongozi katika chumba cha upasuaji katika Hospitali hiyo Bi. Devotha Kimambo, amelipongeza Baraza kwa Mafunzo hayo na kutanabaisha kuwa, yatasaidia kuboresha mazingira ya vyumba vya upasuaji na kuwaongezea ujuzi watumishi wa Taasisi yao.

Nao washiriki wa Mafunzo hayo wamemshukuru Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, kwa jitihada za utoaji wa mafunzo ya aina hiyo kwa watumishi waliopo kazini huku wakiiomba Serikali irudishe mafunzo aina hiyo yaliyositishwa mwaka 2012 ili kuboresha utoaji wa huduma ya usimamizi katika chumba cha upasuaji, ikizingatiwa kuwa Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imejenga Hosiptali za Halmashauri pamoja vituo vingi vya Afya kote nchini zenyesifa ya Kutoa huduma za upasuaji.

Mafunzo hayo yaliyohudhuriwa na wauguzi na wakunga yanatarajiwa kuwa chachu ya utoaji wa huduma bora katika Hospitali ya Mirembe Jijini Dodoma.

Utoaji mafunzo haya ni utaratibu wa kawaida wa Baraza katika kutekeleza majukumu yake ya kuzisimamia taaluma za Uuguzi na Ukunga hapa nchini ili kuhakikisha Jamii inapata huduma bora na salama kupitia Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010.

# Waziri Ummy Awasilisha Mpango wa Bajeti kwa Kamati ya Bunge



***Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya katika  Kamati ya Kudumu ya Bunge.***

***Na Mwandishi wetu.***

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, amewasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya katika kipindi cha Mwezi Julai – Disemba 2023 kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mhe. Stanslaus Nyongo.

Waziri Ummy, amewasilisha taarifa hiyo Januari 17, 2023 ambapo amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuwekeza kwenye Sekta ya Afya na kuboresha Afya za Watanzania.

Waziri Ummy amesema Serikali imewekeza kwenye miundombinu ya kutolea huduma za Afya, kutenga na kutoa Fedha nyingi kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba, kuajiri pamoja na kusomesha wataalam hivyo deni lililobaki ni ubora wa huduma.

“Wizara ya Afya itaelekeza nguvu nyingi katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za Afya ikiwemo matibabu kutoka kwa wataalam waliopo kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya nchini nzima.” Amesema Waziri Ummy

Aidha, amesema kuwa, kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye Sekta ya Afya, Wizara itajielekeza zaidi katika kuboresha huduma za Afya nchini na kuvutia utalii wa tiba kutoka Nchi za Jirani na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha huduma za matibabu ya kibingwa katika ukanda wa Afrika ya Mashariki.

Waziri Ummy Mwalimu, ameambatana na Naibu Waziri wa Afya Mhe. Godwin Mollel, Katibu Mkuu Dkt. John Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Magembe, Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu, Wakurugenzi kutoka Wizara ya Afya pamoja na Wakurugenzi wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

# Lifahamu Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania



***Na Ndimmyake Mwakapiso.***

**SEHEMU YA PILI;**

Katika muendelezo wa Makala hii kwa mwezi huu wa Januari tutaangazia uwepo wa cheo cha Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini.

**UTEUZI WA MSAJILI**

Kwa Mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010; inabainisha kwamba, kutakuwa na Msajili wa Baraza ambaye anateuliwa na Waziri wa Afya, mteule wa nafasi hii ni sharti atoke miongoni mwa watumishi wa umma ambao ni wauguzi au wakunga waandamizi waliosajiliwa, Msajili wa Baraza ndiye atakuwa katibu wa Baraza na Afisa Mtendaji Mkuu.

**MAJUKUMU YA MSAJILI**

Majukumu ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga ni kama ifutavyo;

a) Kusimamia uandikishaji na usajili wa wauguzi na wakunga kwa mujibu wa maealekezo ya Baraza

b) Kuhifadhi na kuimarisha rejista na orodha ya wauguzi na wakunga.

c) Kufanya mabadiliko muhimu na maboresho kwenye rejista na orodha kuhusiana na mabadiliko kwa mujibu wa maelekezo ya Baraza

d) Kukagua na kuweza kuingia kwenye vituo vya huduma za uzazi, vituo vya Uuguzi na Ukunga, Kliniki na shule za mafunzo ya Uuguzi na Ukunga kwa niaba ya Baraza.

e) Kuandika Muhtasari na mwenendo wa vikao vya Baraza na kamati zake zote na atakuwa mtunzaji wa nyaraka zote za Baraza na kamati zake.

f) Kutunza vitabu vya hesabu na mali, kuandaa makadirio ya mwaka na ya ziada pamoja na vitabu vinavyoonesha taarifa za Fedha.

g) Kutekeleza Maamuzi ya Baraza

h) Kutekeleza majukumu engine kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga au yanayoweza kuagizwa na Baraza kwa mujibu wa Sheria.

**USAJILI NA UTOAJI LESENI**

Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga, Baraza litaanzisha, litatunza na kuboresha rejista na orodha ya wauguzi na wakunga wenye sifa, rejista au orodha ya wauguzi na wakunga itakuwa na majina, anuani, sifa na taarifa nyingine za wauguzi na wakunga wote wanaostahili kusajiliwa.

**Sifa za kusajiliwa kwa Muuguzi au Mkunga**

Kwa kuzingatia Sheria ya Uuguzi na Ukunga, mtu yeyote anakuwa na sifa za kusajiliwa kama Muuguzi au Mkunga iwapo mtu huyo;

- Amefaulu mtihani wa Uuguzi na Ukunga iliyoendeshwa na Baraza
- Ametimiza vigezo vingine vya nyongeza kuhusiana na kupata uzoefu katika Uuguzi au Ukunga kadiri Baraza litakavyoona inafaa.
- Amewasilisha ushahidi utakaoridhisha Baraza kwamba amesajiliwa au ana sifa na kuendelea kuwa na sifa za kusajiliwa kama Muuguzi au Mkunga kwenye Nchi yoyote kwa wakati huo kama ilivyoainishwa kwenye kanuni zilizotengenezwa.

*Mkala haya yataendelea Mwezi Februari kwa sehemu ya tatu*

# TANZIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga limepokea kwa masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele za haki Mwezi wa 01 mwaka 2024, baada ya kumaliza kazi yao  hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao mahali pema Peponi AMENI.



**JINA: HILDA OFORO MAFOLE**
**NGAZI :** Hospitall ya Rufaa.
**MKOA :** Kilimanjaro
**WILAYA :** Moshi Mji.



**JINA: ELIZABETH JOHN MOTTO**
**NGAZI :** Hospitall ya Rufaa (Kitete)
**MKOA :** Tabora
**WILAYA :** Tabora Mji



**JINA: AHAZY ANDREW KIPIMILO**
**NGAZI :** Hospitall ya wilaya
**MKOA :** Mbeya
**WILAYA :** Rungwe



**JINA: JOYCE DIKSON**
**NGAZI :** Hospitall ya Rufaa (Msoma)
**MKOA :** Mara
**WILAYA :** Musoma Mji.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGATANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA YA MAHAFALI YA KUMI KWA WAUGUZI NA WAKUNGA

**02.02.2024, Dodoma.**

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania anawaarifu Wahitimu wote wa Kozi za Uuguzi na Ukunga waliofanya Mtihani wa Usajili na Leseni tarehe 29/12/2023 kuwa, Mahafali ya kutoa Vyeti vya Usajili na Leseni yatafanyika siku ya Ijumaa tarehe **23/2/2024** kuanzia **Saa1:00 Asubuhi** katika Ukumbi uliopo katika Kanisa Katoliki la **Mtakatifu Petro - Swaswa** Jijini - Dodoma.

**MADA: -**

Mada mbalimbali zitatolewa ikiwemo, Lijue Baraza la Uuguzi na Ukunga na majukumu yake, Sheria ya Uuguzi Ukunga pamoja na Maadili ya Uuguzi na Ukunga Pamoja na majadiliano mbalimbali yahusuyo taaluma ya Uuguzi na Ukunga.

Washiriki wote mnatakiwa kuthibitisha ushiriki wenu kwa kujaza fomu ya Mahafali kupitia Tovuti ya Baraza la Uuguzi na Ukunga **www.tnmc.go.tz**.

Aidha, mnaelekezwa kuwa, washiriki wote mtatakiwa kuvaa Sare ya Kitaaluma ***"Professional Uniform"*** iliyoidhinishwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga kama ifuatavyo: -

1. **WANAWAKE-** Magauni au Suruali na Blauzi rangi nyeupe ndefu.
2. **WANAUME-** Kaunda Suti- Shati jeupe na suruali dark blue
3. **VIATU**- Vinavyofunika miguu na siyo vya wazi, viwe vya rangi nyeusi, nyeupe au brown.
4. Kitambulisho cha ***Indexing Card*** na kwa wale ambao hawakupata waje na kitambulisho cha NIDA.

**NB: Sandozi au Kandambili haviruhusiwi.**

Kwa mawasiliano zaidi piga namba 0655035078 na 0762003800

Agnes Mtawa
**MSAJILI**

Kambarage Tower, 5th Floor, Benjamin Mkapa Road, P.O. Box 1736, DODOMA Tell: +255262966061/62/63, Mob : +255737 962 691, Email : info@tnmc.go.tz, Website : www.tnmc.go.tz

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA
TANZANIA TOLEO NO 04

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
P.O BOX1736 DODOMA ,TEL.022-212133975
Fax.022-2133975,Email:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI  ZOTE ZIMEHIFADHIWA